
UFUNUO 1

COMIC BIBLE
SOCIETY

Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2023

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


NI MWAKA A.D. 95. - MIAKA SITINI TANGU KIFO NA KUFUFUKA KWA YESU KRISTO.


MTUME PETERO AMESULUBIWA HUKO ROMA - WENGI WASEMA ALISULUBIWA JUU CHINI.
SIFAI KUSULUBIWA NJIA MOJA NA BWANA WANGU YESU.
UNAVYOPENDA.


MTUME PAULO AMEKATWA KICHWA
AKITESWA CHINI YA NERO.


MTUME YOHANA ATUPWA NDANI YA
DEBE LA MAFUTA YANAYOCHEMKA -
LAKINI ABAKI HAI KWA MIUJIZA.



MFALME MPYA AMECHUKUA KITI CHA ENZI.
JINA LAKE NI DOMITIAN - NA KAMA WAFALME WENGI MBELE YAKE - HANA HURUMA.
KARIBUNI ANATEKELEZA DOMINUS ET DEUS - DHEHEBU LA KUABUDU KWA MFALME.
WATU WOTE WANAFAA KUTOA UBANI NA KUKIRI HADHARANI KUWA MFALME NI MUNGU.
--LAKINI KUNDI MOJA LILIKATAA KATU KUFANYA HIVI.
ISALIMISHE – SASA!
YESU KRISTO PEKE YAKE NDIYE MUNGU.
MPELEKE UWANJANI - ATAKIRI HUKO - KWA SIMBA.
ATAULIWA KWA TENDO HILI LA USALITI.


KIFO KWA WAKRISTO
NDIO WANASTAHILI - WAJINGA KWA KUAMINI KUWA MFU SASA AMEFUFUKA.
MAELFU YA WAFUASI WA YESU WAULIWA KAMA TAMASHA KWENYE UWANJA MAARUFU.
KITU KIBAYA KINACHOTENDEKA - IWE NJAA, TAUNI, MTETEMEKO WA ARDHI - MFALME AWALAUMU WAKRISTO.


LAKINI UKOSEFU WA VIONGOZI WALA MATESO NA SERIKALI VINAWEZA KUZIMA IMANI YA WAFUASI HAWA WA KRISTO.
IDADI YA WAFUASI WA KRISTO YAENDELEA KUKUA TU.


KWA KUJARIBU KUSIMAMISHA HARAKATI HII MFALME DOMITIAN AAMUA KUMTOA KIONGOZI WAO YOHANA - MWANAFUNZI WA MWISHO WA YESU ALIYE HAI.


MFALME ANAMHAMISHA YOHANA KWENYE KISIWA CHA PATMO PWANI MWA UGIRIKI. KUTOKA HAPO ANAAMINI KUWA YOHANA HAWEZI TENA KUONGOZA AU KUWASHAWISHI WAKRISTO.


UHAMISHONI PATMO - YOHANA ANAISHI KATIKA PANGO NA ANANGOJA KIFO - AMA KURUDI KWA YESU KULIKO AHIDIWA.
LAKINI NI HAPA KWA KISIWA HIKI KILICHOTENGWA NA KUPIGWA UPEPO KRISTO ALIJIFUNUA YEYE - NA YAJAYO KWA BINADAMU - KWA MTUME YOHANA.
KATIKA NDOTO YA KIUNGU, MUNGU AFUNGUA PAZIA YA YAJAYO NA KUMFUNULIA MTUME UZEENI MWAKE MWISHO MKUBWA WA HADITHI YA BIBILIA...
...KITABU CHA MWISHO CHA BIBILIA - KITABU CHA UFUNUO.






UFUNUO 1:10, 12-17





UFUNUO 1:3, 17-19



KWA YULE ANAYETUPENDA...


...NA KUTUWEKA HURU KUTOKA DHAMBI ZETU KWA DAMU YAKE...


...NA KUTUFANYA TUWE UFALME NA MAKUHANI KUMTUMIKIA MUNGU NA BABA YAKE - KWAKE UWE UTUKUFU NA UWEZO MILELE NA MILELE.


YOHANA, KWA MAKANISA SABA YALIYOKO ASIA:
NEEMA NA AMANI IWE KWENU ZITOKAZO KWAKE YEYE ALIYEKO, NA ALIYEKUWAKO NA ATAKAYEKUJA...


KRISTO AMPATIA YOHANA UJUMBE WA KILA KANISA HASA, LAKINI UJUMBE PIA NI WA MAKANISA YOTE KWA ENZI ZA KANISA.
EFESO ILIKUWA NA BANDARI KUBWA ZAIDI ASIA NA NJIA NNE ZA BIASHARA ZILIPITA KATIKATI YA MJI.
MJI ULIKUWA HEKALU YAKE ILIKUWA MOJA YA MAAJABU SABA YA ULIMWENGU WA KALE.
MTUME PAULO ALIKUWA AMELIANZISHA KANISA. TIMOTHEO NA MTUME YOHANA WOTE WALIHUDUMU HAPO.
KANISA LA EFESO LILIKUWA LIMEBAKIA NA MAFUNDISHO THABITI LAKINI LILIKOSA UPENDO.
NAJUA MATENDO YAKO, BIDII YAKO NA SABURI YAKO.
ILA NINA NENO JUU YAKO - UMEUACHA UPENDO WAKO WA KWANZA.
TUBU UAYATENDE MATENDO YA KWANZA.
KWA WOTE WANAOSHINDA NAWAPA HAKI YA KULA KUTOKA KWA MTI WA UZIMA UNAOPATIKA-NA KATIKA PARADISO YA MUNGU.



SMIRNA (AMBAYO SASA NI IZMIR) ILIKUWA KASKAZINI MWA EFESO NA TAJI LA ASIA - MJI MZURI ZAIDI.
UKIKUWA KITUO CHA SAYANSI NA DAWA - UAMINIFU MKALI KWA ROMA ULITENGENEZA DHEHEBU KALI LA KUABUDU MFALME.
WARUMI NA WAYAHUDI WOTE WALIWA-CHUKIA WALIOMFUATA KRISTO.


KWA HIYO - UKO MZURI SANA KUTOA UBANI KWA MFALME WETU!
TUTAKUONYESHA TUNAVYOFANYA UTOAMINIFU KWA MFALME WA KWELI.
PELEKA TAKATAKA GEREZANI - MUACHE AISHI NA PANYA WENGINE! TUONE VILE AMBAVYO JAMII YAKE ITAISHI MIEZI KADHAA BILA MAPATO.
"NAJUA MATESO NA UMASKINI WAKO - INGAWA U TAJIRI!"
"USIOGOPE MATESO UNAYOENDA KUPITIA."
"KUWA MUAMINIFU MPAKA KWA KIFO, NA NITAKUPA TAJI LA UHAI."
"ANAYESHINDA HATAUIMIZWA HATA NA KIFO CHA PILI."





UFUNUO 2:12-17


KANISA YA THIATIRA ILIKUWA NA MWANAMKE "NABII" ALIYESEMA WATU WALIWEZA KUFANYA UASHERATI BILA KUIDHURU ROHO.
TAJI LA MUNGU KWAKE ILIKUWA KITANDA JEHANAM.
"NITAMUEKA KATIKA KITANDA CHA MATESO NA NITAFANYA WANAOFANYA UZINZI NAYE WATESEKE MNO."
KWA WAFUASI WAKE WALIOTETEA UCHAFU HUO HUO...
"PIA NITAWAUA WATOTO WAKE."
"KWA YULE ANAYESHINDA NA KUFANYA MAPENZI YANGU HADI MWISHO NITAMPA MAMLAKA JUU YA MATAIFA..."


KANISA HUKO SARDI ILIKUWA IMEKUFA - IMEJAWA NA WATU WASIOZALIWA UPYA.
"MNAJULIKANA KWA KUWA HAI - LAKINI MUMEKUFA."
"AMKA!"
"TIA NGUVU KILICHOBAKI NA KI KARIBU KUFA..."
"MSIPOAMKA, NITAKUJA MWENYEWE KAMA MWIZI, NA HAMTAJUA WAKATI GANI NITAKUJA KWENU."
KUNA WATU WACHACHE SARDI AMBAO HAWAJAYACHAFUA MAVAZI YAO."
WATATEMBEA NAMI, WAMEVAA VAZI JEUPE, KWANI WANASTAHILI.
ATAKAYESHINDA ATAKUWA KAMA WAO, ATAVAA NYEUPE.
"NITAHAKIKISHA JINA LAKE HALIFUTWI KUTOKA KWA KITABU CHA UZIMA LAKINI NITADHABITI JINA LAKE MBELE YA BABA YANGU NA MALAIKA."


KANISA LA SITA, FILADELFIA, LILIKUWA KANISA LILOWEKA IMANI.
HUNA HAKI YA KUSEMA HIVYO! TWAJUA YA KWAMBA MUNGU ALIMPA MUSA SHERIA!
LAKINI YESU NDIYE UTIMILIFU WA SHERIA - NA AMBAYE MANABII WETU WALITABIRI.
MUONDOENI! NI MMOJA WA WALE WAFUASI WA KRISTO! WAMALIZE KUTOKA JIJI LETU.
NAJUA UNA NGUVU KIDOGO. BALI UMEWEKA NENO LANGU NA HUJALIKANA JINA LANGU.
"KWA WALE AMBAO NI WA SINAGOGI YA IBILISI, WANAODAI NI WAYAHUDI BALI NI WAONGO..."
"...NITAWAFANYA WAJE NA KUANGUKA MIGUUNI PENU NA KUKIRI KUWA NIMEWAPENDA."
"KWA YULE ANAYESHINDA NITATENGENEZA NGUZO KATIKA HEKALU YA MUNGU WANGU."
"HATAWAHI KUIWACHA TENA..."


KWA MCHUNGAJI WA KANISA LA LAODIKIA KRISTO ALIYAWEKA MANENO YAKE MAKALI ZAIDI...
MJI WA KARIBU WA HIERAPOLIS ULIJULIKANA KWA MASIKA ZA JOTO ILHALI MJI WA KARIBU WA KOLOSSE ULIJULIKANA KWA MASIKA YA BARIDI.
LAKINI LAODIKIA ILIKUWA NA MAJI MACHAFU VUGUVUGU KUTOKA KWA MFEREJI ULIOKUWA CHINI YA ARDHI ULIOSABABISHA WAGENI KUYATEMA PUNDE TU WALIVYOYANYWA.
PTHOO!!
"NAJUA HAMKO MOTO WALA BARIDI - KWA SABABU MUKO VUGUVUGU NITAWATEMA KUTOKA KWA MDOMO WANGU."
MJI ULIKUWA MOJAWAPO WA MIJI TAJIRI ZAIDI KATIKA ENEO HILO NA KUJULIKANA KWA VIWANDA VITATU...
"USHAURI WANGU NI MNUNUNUE DHAHABU KUTOKA KWANGU ILIYOSAFISHWA MOTONI, ILI MUWE MATAJIRI HASA NA MAVAZI MEUPE MVAE KUFINIKA AIBU YA UCHI WENU..."
...DAWA, HASA DAWA YA MACHO.
"MAFUTA YA KUPAKA MACHONI ILI UWEZE KUONA."
"KWA YULE ANAYESHINDA NITAMPA HAKI YA KUKAA NAMI KATIKA KITI CHANGU VHA ENZI, VILE AMBAVYO NILISHINDA NA KUKAA NA BABA YANGU KWA KITI CHAKE CHA ENZI."


BAADA YA KUUFIKISHA UJUMBE WA KRISTO KWA KANISA ZOTE YOHANA APEWA UONO WA MBINGUNI...NA SIKU ZA MWISHO YA DUNIA.
"BAADA YA HIVI NILITAZAMA NA HAPO MBELE YANGU ULIKUWA MLANGO UMESIMAMA WAZI MBINGUNI."
"SAUTI NILIYOISIKIA ILINIONGELE-SHA KWA MARA NYENGINE, 'NJOO HAPA JUU NA NITAKUONYESHA KITAKACHOFANYIKA BAADA YA HIVI.'"
"MARA MOJA NIKAWA NDANI YA ROHO, NA HAPO MBEE YANGU KULIKUWA NA KITI CHA ENZI MBINGUNI NA MTU AMEKIKALIA."


"NAYE ALIYEKETI HAPO ALIONEKANA MITHILI YA JIWE LA YASPI NA AKIKI."
"...UPINDE WA MVUA ULIKIZUNGUKA KILE KITI CHA ENZI, UKIONEKANA MITHILI YA ZUMARIDI..."
"KULIKUWA NA VITI VYENGINE ISHIRINI NA VINNE VYA ENZI..."
"...MBELE YA KITI CHA ENZI TAA SABA ZILIWAKA..."
UFUNUO 4:1


"NA KATIKATI YA KILE KITI CHA ENZI, NA PANDE ZOTE ZA KILE KITI, WALIKUWAKO WENYE UHAI WANNE. [1] WALA HAWAPUMZIKI MCHANA WALA USIKU, WAKISEMA, MTAKATIFU, MTAKATIFU, MTAKATIFU, BWANA MUNGU MWENYEZI, ALIYEKUWAKO NA ALIYEKO NA ATAKAYEKUJA. "


[1] VIUMBE HAWA WAMEJAWA NA MACHO. HAWAJUI YOTE - MUNGU PEKE YAKE NDIYE ALIYE HIVYO. LAKINI VIUMBE HAWA WANA MAARIFA NA MAONO MAPANA.
UFUNUO 4:6-8


"NA HAO WENYE UHAI WANAPOMPA YEYE AKETIYE JUU YA KITI CHA ENZI UTUKUFU, NA HESHIMA, NA SHUKRANI, YEYE ALIYE HAI HATA MILELE NA MILELE NA ANAYEISHI MILELE, NDIPO HAO WAZEE ISHIRINI NA WANNE HUANGUKA MBELE ZAKE YEYE AKETIYE JUU YA KILE KITI CHA ENZI, NAO HUMSUJUDIA YEYE ALIYE HAI HATA MILELE NA MILELE."


UNASTAHILI E BWANA NA MUNGU, KUPOKEA UTUKUFU NA HESHIMA NA UWEZO, KWANI ULIUMBA VITU VYOTE NA KWA NIA YAKO VILIUMBWA NA VINA UWEPO.




[1] INAWEZEKANA HII NI HATI MILIKI YA ARDHI. KAMA HATI RASMI ZA KIRUMI - ILIKUWA NA MUHURI SABA.


"NIKAONA MWANA-KONDOO AMESIMAMA, ALIKUWA KANA KWAMBA AMECHINJWA, KASIMAMA KATIKATI YA KITI CHA ENZI, KAZUNGUKWA NA NA WALE WENYE UHAI WANNE, NA WALE WAZEE."


"ALIKUWA NA PEMBE SABA NA MACHO SABA, AMBAZO NI ROHO SABA ZA MUNGU ZILIZOTUMWA KATIKA DUNIA YOTE."


"AKAJA, AKAKITWAA KILE KITABU KATIKA MKONO WA KUUME WAKE YEYE ALIYEKETI JUU YA KILE KITI CHA ENZI."
"HATA ALIPOKITWAA KILE KITABU, HAO WENYE UHAI WANNE NA WALE WAZEE ISHIRINI NA WANNE WAKAANGUKA MBELE ZA MWANA-KONDOO."
"KILA MMOJA WAO ANA KINUBI, NA VITASA VYA DHAHABU VILIVYOJAA MANUKATO, AMBAYO NI MAOMBI YA WATAKATIFU."
NAO WALIIMBA WIMBO MPYA WAKISEMA...
WASTAHILI WEWE KUKITWAA HICHO KITABU NA KUZIFUNGUA MUHURI ZAKE, KWA KUWA ULICHINJWA, UKAMNUNULIA MUNGU KWA DAMU YAKO WATU WA KILA KABILA NA LUGHA NA JAMAA NA TAIFA.



UFUNUO 5:7-9


UKAWAFANYA KUWA UFALME NA MAKUHANI WA KUMTUMIKIA MUNGU WETU...NAO WATAMILIKI JUU YA NCHI.
YOHANA BASI ANAWAKILISHA PICHA YA KWAYA YA MALAIKA AMBAYO ULIMWENGU HAUJAPATA KUONA - IDADI YAKE KWAYA HIYO IKO KATIKA MAMILIONI.
ASTAHILI MWANA-KONDOO ALIYECHINJWA, KUUPOKEA UWEZA NA UTAJIRI NA HEKIMA NA NGUVU NA HESHIMA NA UTUKUFU NA BARAKA!


"NA NIKASIKIA KILA KIUMBE MBINGUNI..."
"...NA NCHINI NA CHINI YA NCHI..."
"...NA JUU YA BAHARI, NA VITU VYOTE VILIVYOMO NDANI YAKE VIKIIMBA..."
BARAKA NA HESHIMA NA UTUKUFU NA UWEZA UNA YEYE AKETIYE JUU YA KITI CHA ENZI, NA KWA MWANA-KONDOO, HATA MILELE NA MILELE.
UFUNUO 5:13


AMINA.
AMINA.
AMINA.




[1] FARASI MWEUPE ANAWAKILISHA WAKATI WA AMANI ULIMWENGUNI USIYO NA KIFANI. LAKINI HII NI AMANI KUPITIA MASSIAH WAONGO, KILELE KIKIWA MPINGA KRISTO. ULIMWENGU MZIMA UTAMFUATA HUYU ALIYEPANDA FARASI, NA NIA YA KUIPATA AMANI HII YA UONGO.

[2] UPINDE NI ISHARA YA VITA, LAKINI KUTOKUWEPO KWA MISHALE YAWEZA KUWA INAMAANISHA AMANI ILIPATIKANA KWA AGANO WALA SIO KWA VITA.


"NIKATAZAMA, NA HAPO MBELE YANGU ALIKUWEPO FARASI MWEUPE." [1]
"ALIYEMPANDA ALISHIKILIA UTA, AKAPEWA TAJI NAYE AKATOKA KAMA MSHINDI ALIYE NA INADI KUSHINDA." [2]
VOTE
UFUNUO 6:1-2


"NA MWANA-KONDOO ALIPOIFUNGUA MUHURI WA PILI, NIKAMSIKIA YULE MWENYE UHAI WA PILI AKISEMA, 'NJOO!'"
"AKATOKA FARASI MWINGINE, MWEKUNDU SANA KAMA MOTO."
[1] SASA JANGA LA VITA NA VURUGU LITASHUKA ULIMWENGUNI.
NI MWANZO WA UCHUNGU WA UZAZI ULIOELEZWA NA KRISTO ALIPOFUNZA HAPA ULIMWENGUNI.
NI WAKATI AMBAPO KUCHINJA KWA UKATILI UTAKUWA KAWAIDA.
KUTAKUWA NA UASI, UAJI, MAUAJI NA KUENEA KWA UMWAGAJI WA DAMU.


"NAYE ALIYEMPANDA ALIPEWA KUIONDOA AMANI KATIKA NCHI, ILI WATU WAUANE." [1]
"NAYE AKAPEWA UPANGA MKUBWA."
UFUNUO 6:3


"NA MWANA-KONDOO ALIPOIFUNGUA MUHURI YA TATU, NIKAMSIKIA YULE WA TATU MWENYE UHAI AKISEMA, 'NJOO!'"
KIBABA CHA NGANO KWA NUSU RUPIA, NA VIBABA VITATU VYA SHAYIRI KWA NUSU RUPIA, WALA USIYADHURU MAFUTA WALA DIVAI. [2]
[1] VITA ULIMWENGUNI VITAKATIZA USAMBAZAJI WA CHAKULA NA KULETA MAJANGA YA NJAA ULIMWENGUNI. MIZANI YAONYESHA KUWA UKOSAJI WA CHAKULA UTALETA KUGAWA KWA CHAKULA NA FOLENI ZA CHAKULA.
[2] KIASI KINAONYESHA WATU WATAFANYA KAZI SIKU NZIMA KWA CHAKULA CHA SIKU HIYO TU. SHAYIRI AMBAYO KAWAIDA HUPEWA WANYAMA, ITALIWA NA BINADAMU. BIDHAA KAMA MAFUTA NA DIVAI ZINAZOTUMIWA KWA UPISHO ZITACHUKULIWA KAMA UTAJIRI.


NIKATAZAMA, NA HAPO MBELE YANGU, FARASI MWEUSI! NAYE ALIYEMPANDA ANA MIZANI MKONONI MWAKE." [1]
"NA NIKASIKIA KAMA SAUTI KATIKATI YA HAO WENYE UHAI WANNE, IKISEMA..."
UFUNUO 6:5


"NA MWANA-KONDOO ALIPOIFUNGUA MUHURI YA NNE, NIKASIKIA SAUTI YA YULE MWENYE UHAI WA NNE AKISEMA, 'NJOO!'"
"NIKATAZAMA, NA HAPO MBELE YANGU, FARASI WA RANGI YA KIJIVUJIVU!" [1]
"NAO WAKAPEWA MAMLAKA JUU YA ROBO YA NCHI, WAUE KWA UPANGA NA KWA NJAA NA KWA TAUNI NA KWA HAYAWANI WA NCHI." [2]
[1] KAMA MATOKEO YA VITA NA NJAA MAGONJWA NA TAUNI ZAIDI YATATOKEA KOTE ULIMWENGUNI.
[2] HATA LEO, MAGONJWA YALIYOANGAMIZWA HAPO AWALI YANARUDI KOTE ULIMWENGUNI. UHARIBIFU UNAOKUJA KAMA MATOKEO YA VITA, NJAA NA MAGONJWA SASA YANAANGAMIZA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA IDADI YA WATU ULIMWENGUNI.


NO HOPE
HUNGRY
"NAYE ALIYEMPANDA JINA LAKE NI MAUTI, NA KUZIMU AKAFUATANA NAYE."





**SUPERBIBLE.TV**